

# **HALMASHAURI YA MJI WA KONDOA**

*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Halmashauri ya Mji wa Kondoaa)*

## **MJI WA KONDOA**

**Simu: +255 262360028**

**Fax: +255 262360028**

Barua pepe :td@kondoatc.go.tz



**Sanduku la Posta 711,  
KONDOA.**

## **TAARIFA YA IDARA YA ELIMU SEKONDARI**

### **1. UTANGULIZI.**

Halmashauri ya Mji Kondoaa ina jumla ya shule za Sekondari (12) kumi na mbili, kati ya hizo (9) tisa ni za Serikali na (3) tatu ni za Binafsi.

Katika shule za Serikali kuna Jumla ya wanafunzi 3830, kwa kidato cha kwanza hadi cha sita kati yao wavulana na 1299 na wasichana ni 2531, shule binafsi zina jumla ya wanafunzi 1042, ambao wavulana ni 407 na Wasichana ni 635 kwa kidato cha kwanza hadi cha nne.

Idara ya Elimu Sekondari ina jumla ya walimu 170, kati yao wanawake ni 66 na wanaume ni 104, hata hivyo Idara ina upungufu wa walimu katika Masomo ya Sayansi.

### **Mawasiliano ya Watumishi na Idara.**

Idara ya Elimu Sekondari ina Jumla ya watumishi wanne na mawasiliano yao ni kama inavyoonekana kwenye jedwali:-

<b>SN</b>	<b>JINA LA AFISA</b>	<b>CHEO</b>	<b>NAMBA YA SIMU</b>
1.	Venance Mwizarubi	Afisa Elimu Sekondari Mji (TSEO)	0765 – 275236 <a href="mailto:Mwizarubi62@gmail.com">Mwizarubi62@gmail.com</a>
2.	Salehe Jengo	Afisa Elimu Vifaa na Takwimu (SLO)	0784 – 337808 <a href="mailto:jengoalfred@gmail.com">jengoalfred@gmail.com</a>
3.	Safi Mturi	Afisa Elimu Taaluma	0685 – 777901

		(TSAO)	<a href="mailto:safikhalifa@yahoo.com">safikhalifa@yahoo.com</a>
4.	Emmanuel Ndee	Afisa Elimu Vifaa na Takwimu Msaidizi (ASS. SLO)	0784 – 242055 <a href="mailto:ndeemm@gmail.com">ndeemm@gmail.com</a>

### **KAZI ZA IDARA.**

Idara ya Elimu Sekondari ndiyo yenyeye dhamana na kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu elimu Sekondari katika Halmashauri ya Mji Kondo. Shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuratibu shughuli zote zinazohusu taaluma katika Halmashauri
- ii. Kusimamia utendaji kazi wa walimu na watumishi wa idara ya Elimu wasio kuwa walimu.
- iii. Kuratibu takwimu zote za Idara ya Elimu kama vile Miundombinu ie vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, n.k, idadi ya wanafunzi, walimu na nyinginezo.
- iv. Kuratibu Maslahi ya walimu kama likizo, madai mbalimbali kama vile uhamisho, mizigo na malimbikizo ya mishahara pamoja na kupanda madaraja.
- v. Ulinzi na usimamizi wa mali za Umma zitumikazo katika Uendeshaji wa Elimu Sekondari kama vile Samani za shule, maeneo ya shule na mali nyingine.
- vi. Kuthibiti utoro wa walimu na wanafunzi na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria, taratibu na Kanuni za Elimu na nchi kwa ujumla.

### **4. HUDUMA ZINAZOTOLEWA.**

Idara ya Elimu Sekondari inatoa huduma mbalimbali zinazohusiana na mambo ya Elimu na Taaluma kwa wanafunzi, wananchi na Walimu kwa ujumla. Vilevile Idara hii hutoa huduma kama inavyoolekezwa na Mkurugenzi wa Halmashauri Katibu Tawala Mkoa na Viongozi mbalimbali wanchi kwa kuzingatia miongozo, nyaraka na maelekezo mbalimbali. Baadhi ya Huduma zitolewazo ni kama ifuatavyo:

- i. Kushughulikia uhamisho wa wanafunzi na walimu
- ii. Kushughulikia likizo za walimu na watumishi na wasio walimu wanaohudumia katika Idara ya Elimu Sekondari.

- iii. Kushughulikia masuala ya kinidhamu na utoro wa walimu na wanafunzi.
- iv. Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wazazi, wanafunzi na walimu kwa ujumla
- v. Maslahi ya walimu kama madaraja n.k
- vi. Huduma mbalimbali zinazohusiana na taaluma.

## **MATARAJIO YA IDARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018.**

Idara inatarajiwa kufanya mambo yafuatayo:

- i. Kupandisha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wanaofanya mitihani ya Taifa kama vile Mitihani ya kidato cha Pili, Nne na Sita.
- ii. Kuamsha ari ari ya utendaji kazi kwa walimu ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi.
- iii. Kujenga uhusiano mzuri baina ya walimu, wanafunzi na Jamii inayozunguka shule (wananchi)
- iv. Kuhakikisha maslahi ya walimu yanaboreshw na kupatikana kwa wakati kama vile fedhs za likizo, uhamisho, kupanda madaraja kwa walimu, makazi bora ya walimu, upatikanaji wa vifaa vyaa kusomea na kufundisha kwa wakati.
- v. Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa Elimu na kuwapatia watoto elimu bora.

## **HITIMISHO.**

Idara ya Elimu Sekondari inatoa rai kwa walimu kufundisha, na kusimamia nidhamu za wanafunzi vilevile tunawaomba wazazi wawape ushirikiano walimu ili kuhakikisha watoto wanapata elimu bora.

- Wanafunzi wajitambue na kujua umuhimu wa Elimu kwao binafsi na kwa Taifa kwa Ujumla.
- Idara ya Elimu Sekondari inatarajia kuitia elimu inayotolewa katika Halmashauri ya Mji Kondoa ili kupata Taifa bora na lenye kujitambua.

Nawasilisha